

HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU
IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA
TAARIFA FUPI YA SEKTA YA KILIMO YA KATA YA MWABUSALU

1. UTANGULIZI

Kata ya Mwabusalu ni miongoni ya kata 29 za Wilaya ya Meatu. Wilayah ii ipo katika Tarafa ya Kisesa na ukanda wa Kaskazini wa kilimo (Nothern Agro-ecological zone).

Kata ya Mwabusalu inaundwa na vijiji 4 ambayo ni; Mwabusalu, Ikigijo, Nzanza na Mwakipugila. Kata hii ina kaya 1,570 zenye jumla ya wakazi 11,891 ambao kati yao wanaume ni 5,723 na Wanawake 6,171. Wastani wa wa idadi ya watu kwa kaya ni 7.6 hii ni kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Kwa kuzingatia kiwango cha wilaya cha ukuwaji wa idadi ya watu (Population growth rate) cha 7.1% kwa mwaka Kata ya Mwabusalu inakadiriwa kuwa na kaya 1,686 zenye jumla ya watu 12,774 ambao kati yao wanaume ni 6,146 na wanawake ni 6,627 kwa sasa. Shughuli kuu ya wakazi wa kata hii ni Kilimo cha mazao mbalimbali ikiwemo Pamba, Viazi vitamu na Mahindi.

2.0 HALI YA KILIMO

Kilimo katika kata hii hufanyika katika mashamba madogomadogo yenye ukubwa wa wastani wa kuanzia ½ ekari hadi ekari 2. Zao la Pamba ndilo linalotegemewa na wakazi wengi wa kata hii. Katika msimu wa kilimo uliopita jumla kilo 2,091,980 za pamba mbegu zilizalishwa katika vijiji vyote vinne vya kata ya Mwabusalu. Kiasi hiki cha pamba kiliwaingizia wakazi mapato ya fedha jumla ya Tsh. 2,091,980,000/- kwa mauzo ya pamba ya wastani wa bei ya Tsh. 1,000/- kwa kilo.

Hata hivyo, uzalishaji wa pamba kwa msimu uliopita uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtawanyiko mbaya wa mvua na uotaji hafifu wa mbegu.

3.0 UZALISHAJI WA MBEGU

Katika msimu huu wa kilimo vijiji vyote vya kata ya Mwabusalu (Mwabusalu, Nzanza, Ikigijo, na Mwakipugila) vimehusishwa kwenye mpango wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba, UKM08.

Utekelezaji wa mpango huu umefuatia utafiti uliofanyika juu ya uwepo wa ugonjwa hatari wa pamba uitwao Mnyauko fuzari “Fusarium wilt” unaosababishwa na vimelea aina ya ukungu “fungus” viitwayo *Fusarium oxysporum fs vesinfectum* na unaenea hasa kwa njia ya mbegu na udongo.

Utafiti ulifanywa kwa ushirikiano na Taasisi za Utafiti wa Kilimo Ukirigulu-ARDI, Maruku-ARDI na halmashauri ya wilaya ya Meatu.

4.0 MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti uliofanyika haukubaini dalili zozote za kuwepo kwa ugonjwa huu wilayani kwetu. Jumla ya mashamba ya pamba 316 katika vijiji 106 yalitembelewa na kukaguliwa katika utafiti huu.

Matokeo haya ya utafiti yameiwezesha wilaya yetu kuwa na sifa ya kuzalisha mbegu bora za pamba. Hivyo, katika msimu huu wa kilimo, Kampuni ya Quton (T) Ltd kwa kushirikiana na Gaki ginning Co. Ltd inatarajia kuzalisha mbegu aina ya UKM08 kupitia wakulima waliopo katika vijiji vya kata ya Mwabusalu.

5.0 MAKUBALIANO JUU YA UZALISHAJI WA MBEGU ZA PAMBA

Makubaliano ya uzalishaji wa mbegu yameanza kufanyika kati ya kampuni ya Quton, Gaki Ginning na Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Randama ya Maelewano (Memorandum of Understanding – MoU) imeshaundwa kwa kushirikiana na pande zote tatu na hatua iliyobaki ni kuwashirikisha wakulima tayari kwa shughuli kuanza. Randama ya maelewano imeambatishwa.

Christopher M. Simwimba
Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
Halmashauri ya Wilaya
MEATU